

Pata majibu kuhusu chanjo ya COVID-19



FDA imeidhinisha chanjo ya Pfizer/BioNTech ya COVID-19 kwa mtu yeyote aliye na umri wa miaka 12 au zaidi. Hii ni hatua ya kutia moyo na muhimu katika mapambano dhidi ya janga hili. **Chanjo ya Pfizer ndiyo chanjo pekee ya COVID-19 iliyoidhinishwa kwa watoto.** Chanjo ya Moderna na Johnson & Johnson/Janssen imeidhinishwa kwa watu wenye umri wa miaka 18 na zaidi.

Chanjo za COVID-19 sio tu fanisi sana katika kuzuia magonjwa, kulazwa hospitalini, na kifo ¹ lakini zitatusaidia kurejelea shughuli zetu za kawaida. Tafti za hivi karibuni zinaonyesha chanjo inafanya kazi dhidi ya aina tofauti za virusi zilizotambuliwa hadi sasa ² na zinazuia maambukizi ya virusi kwa watu wengine. Watu wanaochagua kupata chanjo hawajikingi tu kutokana na virusi, lakini pia wanasaidia kulinda wale katika jamii yetu wanaoweza kuwa katika hatari zaidi ya kuathiriwa na ugonjwa au wasioweza kupata chanjo sasa hivi.



Je, ni lazima nipate chanjo kama tayari nilikuwa na COVID-19?

Ndiyo, hata ikiwa tayari ulikuwa na COVID-19 bado unapaswa kupata chanjo. Chanjo hutoa kinga ya ziada kutokana na ugonjwa na uwezekano wa kuambukizwa tena. Tafti zinaonyesha kuwa chanjo inakuinga vizuri zaidi kutokana na aina tofauti za virusi. Hii inaweza pia kumaanisha kuwa chanjo hutoa kinga ya muda mrefu zaidi ikilinganishwa na kinga ya asili, au kinga kutokana na kuwa na ugonjwa. Chanjo ni njia salama na bora zaidi ya kukuza kinga kuliko kuambukizwa na virusi na kuwa na COVID-19 kama ugonjwa.

Je, ninaweza kupata athari gani baada ya kupata chanjo?³

Chanjo ya COVID-19 ni salama na yenye ufanisi. Lakini, kama dawa zote, baadhi ya watu wanaweza kuwa na athari, kwa hivyo ni muhimu kufahamu athari hizi na ishara za kuangalia.

Athari za kawaida

Unaweza kuwa na athari nyepesi hadi wastani, kwa siku chache. Hizi ni ishara za kawaida kwamba mwili unajenga kinga na kinga ya mwili inafanya kile inachotakiwa kufanya. Athari hizi kawaida huisha baada ya saa 12-48. Baadhi ya watu hawapati athari zozote au wanaweza kuwa na athari tofauti baada ya dozi yao ya 2 kuliko zile walizopata baada ya dozi yao ya 1. Kupata athari ya kawaida sio sababu ya kukosa kupata dozi ya 2 cha chanjo ya mRNA ya COVID-19. Unahitaji dozi zote mbili ili kulindwa kikamilifu.

¹ <https://www.cdc.gov/vaccines/acip/meetings/downloads/slides-2021-05-12/04-COVID-Oliver-508.pdf>

² <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/science/science-briefs/fully-vaccinated-people.html>

³ <https://www.cdc.gov/vaccines/covid-19/info-by-product/pfizer/reactogenicity.html>

Mkononi katika sehemu iliyodungwa sindano:

- Maumivu
- Wekundu
- Uvimbe

Katika mwili wako wote:

- Kibaridi
- Kuhara
- Homa au kuhisi jasho
- Maumivu ya kichwa
- Maumivu ya misuli
- Kichefuchefu, au kuhisi kuumwa na tumbo
- Uchovu

Athari zisizo za kawaida

Baadhi ya watoto wanaweza kupata uvimbe au ulaini wa vinundu vya limfu (ugonjwa unaoitwa lymphadenopathy), kawaida kwenye eneo la kwapa au shingo.

Baadhi ya watu wanaweza kuwa na upele mwekundu, unaowasha, wenye uvimbe, au maumivu mahali walidungwa, ambao mara nyingi huitwa “upele wa chanjo ya COVID.” Vipele hivi vinaweza kuanza siku chache hadi zaidi ya wiki moja baada ya dozi ya 1. Ikiwa mtoto wako anapata “upele wa chanjo ya COVID” baada ya kupata dozi ya 1, bado anapaswa kupata dozi ya 2. Muulize daktari wa mtoto wako kuhusu kutibu hali hii na dawa za kutibu mizio (antihistamine) ili kusaidia kupunguza mwasho, au acetaminophen au dawa isiyo ya steroidi ya kuzuia uvimbe (NSAID) kwa maumivu.



Vidokezo vya kusaidia kudhibiti athari

Ni vyema zaidi kusubiri kadri ya uwezo wako kabla ya kumeza dawa zozote za kutuliza maumivu baada ya kupata chanjo. Zungumza na daktari wako kuhusu kutumia dawa isiyo na maagizo ya daktari, kama vile ibuprofen, acetaminophen (ambayo mara nyingi huitwa Tylenol), au naprosyn, ili kusaidia kupunguza maumivu au usumbufu kutokana na athari yoyote.

Ni muhimu kuendelea kutumia dawa za kila siku za muda mrefu baada ya chanjo, isipokuwa daktari wako amekueleza vinginevyo.

Ili kupunguza maumivu na usumbufu katika eneo ulilodungwa:

- Wekelea kitambaa safi, chenye baridi, na unyevu kwenye eneo hilo.
- Tumia au uufanyishe mkono wako mazoezi.

Ili kupunguza athari za homa:

- Kunywa maji mengi.
- Vaa nguo nyepesi, ambazo hazitakupa joto jingi



Wakati wa kupigia daktari simu

Katika hali nyingi, utapata athari za kawaida tu. Piga simu kwa daktari au mtoa huduma ya afya:

- Ikiwa wekundu au wororo katika sehemu uliyodungwa utaanza kuongezeka baada ya saa 24 (au siku 1).
- Ikiwa una wasiwasi kuhusu dalili zozote zisizo za kawaida ambazo unaweza kuwa nazo, au una maswali kuhusu mchanganyiko wa athari kutokana na kupata chanjo zaidi ya moja kwa wakati mmoja.
- Ikiwa una wasiwasi kuhusu athari zako au ikiwa athari haziishi baada ya siku chache.

Piga simu daktari mara moja ikiwa una dalili hizi hadi wiki 3 baada ya kupata chanjo ya COVID-19:

- Mapigo ya moyo yasiyo ya kawaida
- Uwezo uliopungua wa kuona
- Maumivu ya kifua
- Kuchanganyikiwa au matatizo ya kuongea
- Kuzimia au kupoteza fahamu
- Uvimbe wa miguu
- Mchubuko mpya au rahisi
- Petechiae (madoa madogo mekundu kwenye ngozi)
- Maumivu makali ya tumbo ambayo hayaishi
- Maumivu makali ya kichwa au maumivu ya kichwa ambayo hayaishi
- Kifafa
- Upungufu wa pumzi
- Udhaifu au mabadiliko ya utambuzi



Athari kali au mbaya baada ya kupata chanjo ni nadra⁴

Athari za mzio zinachukuliwa kuwa kali ikiwa mtu anahitaji kutibiwa na epinephrine au EpiPen® au kwenda hospitalini. Aina hizi za athari huitwa anafleksisi, na karibu kila wakati hutokea ndani ya dakika 30 baada ya kupata chanjo. Watu wanaweza kuwa na matatizo ya kupumua, uvimbe wa uso na koo, mapigo ya moyo ya haraka, upele mbaya mwili mzima, au kizunguzungu na udhaifu. Hii ndio sababu ni muhimu kukaa kwa dakika 15-30 baada ya kupata chanjo, ili daktari wako aweze kuangalia na kuhakikisha kila kitu ni sawa. Dawa zinapatikana kutibu anafleksisi. Mtu yeyote ambaye ana athari ya anafleksisi baada ya dozi ya 1 ya chanjo **hapaswi** kupata dozi ya 2.

Athari zisizo kali, za baada ya muda mfupi za mzio pia ni nadra.

Athari za mzio ambazo hazihitaji huduma ya dharura au kulazwa hospitalini huitwa athari za mzio zisizo kali. Aina hizi za athari hutokea ndani ya saa 4 baada ya kupata chanjo. Watu wanaweza kupata mabaka, uvimbe au kukorota. Ikiwa mtoto wako ana athari zisizo kali za mzio baada ya kupata dozi ya chanjo ya COVID-19 hapaswi kupata dozi ya 2, hata ikiwa athari haikuwa kali vya kutosha kuhitaji huduma ya dharura au kulazwa hospitalini.



⁴ <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/safety/allergic-reaction.html>

Uwezekano wa athari ya muda mrefu ni mdogo sana.

Ukiangalia historia ya chanjo zote, idadi kubwa ya athari za muda mrefu kutokana na chanjo hutokea kati ya siku 30-45 baada ya majaribio ya kimatibabu ya chanjo kumalizika. Ndiyo sababu FDA inahitaji muda wa kusubiri wa angalau siku 60 baada ya kumalizika kwa jaribio la kimatibabu kabla ya idhini ya matumizi ya dharura (EUA) kutolewa.

FDA na CDC zitaendelea kufuatilia athari nadra yoyote inayowezekana

Chanjo zilitengenezwa haraka kwa kuondoa taratibu za kawaida na urasimu, bila kuchukua njia za mkato au kuruka tahadhari yoyote ya usalama. Wanasayansi wamekuwa wakifanya kazi na teknolojia iliyotumiwa kutengeneza chanjo hizi kwa zaidi ya muongo mmoja. Mamilioni ya visa vya COVID-19 kote ulimwenguni viliwezesha wanasayansi kuchunguza haraka virusi ili kutengeneza chanjo iliyokuwa salama na yenye ufanisi. Mamilioni ya watu nchini Marekani wamepokea chanjo za COVID-19 chini ya ufuatiliaji mkali zaidi wa kiusalama katika historia. FDA, CDC, na Kamati ya Ushauri ya Desturi za Chanjo (ACIP)⁵ wamekagua kwa uangalifu data yote inayopatikana na wana uhakika chanjo ni salama na yenye ufanisi kuzuia COVID-19. **Uwezekano wako wa kuwa na hali ya kutishia maisha ya COVID-19 ni kubwa zaidi kuliko hatari yako ya kupata athari kali kutokana na chanjo.**



Marekani ina mfumo bora zaidi ulimwenguni⁶ wa kuchunguza athari nadra zinazoweza kupatikana tu wakati chanjo zinatolewa zaidi kwa watu wengi. CDC inaripoti kwa umma kila wakati mtu anaporipoti maradhi baada ya kupata chanjo, iwe ugonjwa unasababishwa na chanjo au la. Mtu yeyote anaweza kuripoti maradhi au athari kali baada ya kupata chanjo, sio tu madaktari. Taarifa hii inaripotiwa kupitia Mfumo wa Kuripoti Tukio Baya la Chanjo (VAERS). Ni muhimu kukumbuka kuwa ikiwa tatizo la kiafya limeripotiwa kwa VAERS, hiyo haimaanishi kuwa tatizo lilisababishwa na chanjo. Inaonya tu wanasayansi, wataalam wa usalama wa chanjo, na madaktari kuhusu matatizo yoyote yanayowezekana yanayoweza kuhitaji kuchunguzwa kwa uangalifu zaidi.

Mfano wa jinsi mfumo unavyofanya kwa ufanisi ilikuwa kugundua haraka sana kwamba chanjo ya Johnson & Johnson ya COVID-19 ilihusishwa na aina nadra sana ya kuganda kwa damu (mvilio kwenye mishipa ya damu au thrombosis na ugonjwa wa idadi ndogo ya vigandisha damu(thrombocytopenia) au TTS) ambayo inahitaji kutibiwa tofauti na aina zingine za kuganda kwa damu. Mfumo wa VAERS uliweza kutambua athari hii nadra na CDC iliweza kujulisha madaktari njia bora ya kutibu aina hii ya kuganda kwa damu. Sasa, hata ikiwa mtu atapata athari hii nadra, madaktari wanaweza kuitibu. Ni muhimu kutaja kuwa chanjo ya Johnson & Johnson ni aina tofauti ya chanjo kuliko chanjo za mRNA za Pfizer na Moderna. Hakujakuwa na uhusiano wowote na kuganda kwa damu katika dozi zaidi ya milioni 200 za chanjo za Pfizer na Moderna. Chanjo ya Pfizer ndiyo chanjo pekee ya COVID-19 iliyoidhinishwa kwa watoto.

Mfumo wa usalama wa chanjo umepokea baadhi ya ripoti kuhusu myocarditisi (uvimbe na uvimbe unaotokana na kinga wa misuli ya moyo) au pericarditisi (uvimbe kwenye utando unaozunguka moyo).⁷ Hali hizi za kiafya ni kawaida. Myocarditisi na pericarditisi kawaida hutokea baada ya kuambukizwa na virusi kama vile homa, ugonjwa wa Lyme, au hata COVID-19, na zinaweza kutibiwa. Karibu watu 10 hadi 20 kati ya kila watu 100,000 katika Marekani wanatambuliwa na myocarditisi kila mwaka. Haijulikani bado ikiwa hali hizi nadra za myocarditis zinahusishwa na chanjo. Hivi karibuni Shirika la Moyo la Marekani lilitoa taarifa⁸ kuwashauri watu kwamba kwa kuwa visa vilivyoripotiwa ni nadra na haswa ni vyepesi, manufaa ya chanjo za COVID-19 bado yanazidi hatari yoyote inayoweza kutokea ya athari hii.

5 https://www.cdc.gov/mmwr/volumes/70/wr/mm7020e1.htm?s_cid=mm7020e1_w

6 <https://www.cdc.gov/vaccinesafety/index.html>

7 <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/safety/myocarditis.html>

8 <https://newsroom.heart.org/news/covid-19-vaccine-benefits-still-outweigh-risks-despite-possible-rare-heart-complications>

Je, kwa nini watoto wanahitaji kupata chanjo ya COVID-19?

Kuna kutokuelewana kwa kawaida kwamba watoto hawawezi kupata COVID-19 au hawana hatari ya kupata maradhi makali kutokana na virusi. Hata hivyo, baadhi ya watoto wanaugua sana na kuhitaji matibabu hospitalini. Kuna mengi ambayo bado hatujui kuhusu jinsi COVID-19 itaendelea kuathiri watoto kwa muda mrefu.

COVID-19 ni hatari zaidi kuliko hatari zozote zinazoweza kutokana na kupata chanjo. Watoto wanakabiliwa na athari kali, zinazoweza kudumu kwa kiwango sawa na watu wazima, hata wakati hawajakuwa na dalili au walikuwa na dalili nyepesi tu wakati wa maambukizi yao. Watoto wengi wanaendelea kuathiriwa kutokana na uchovu, maumivu ya kichwa, maumivu ya tumbo, maumivu ya misuli na viungo, na ugumu wa kumbukumbu na uchakataji wa maelezo.

Tangu mwanzo wa janga, watoto 77,827 wa Utah wenye umri wa miaka 0-18 wamepatikana na COVID-19, na 683 walihitaji kulazwa hospitalini. Kati ya wale waliohitaji kulazwa hospitalini katika kikundi hicho cha umri, 74 walipata ugonjwa wa uvimbe wa viungo vingi kwa watoto (MIS-C). MIS-C ni tatizo baya ambalo linaweza kusababisha kifo.



Je, chanjo za COVID-19 zimesababisha vifo vyovyote?

Hakujakuwa na vifo vilivyosababishwa moja kwa moja na chanjo, kati ya dozi zaidi ya milioni 259 za COVID-19 zilizotolewa Marekani kuanzia tarehe 14 Disemba 2020 hadi tarehe 10 Mei 2021.⁹

CDC iligundua kuwa chanjo ya Johnson & Johnson COVID-19 ilisababisha tukio nadra na kubwa na kali — kuganda kwa damu yenye idadi ndogo ya vigandisha damu—kwa idadi ndogo sana ya watu. Wakati huo, madaktari wengi hawakufahamu kuwa kuganda huku nadra kwa damu kunahitaji kutibiwa tofauti na vile wangeweza kutibu kuganda kwingine kwa damu. Kwa bahati mbaya, kutibu kuganda huku nadra kwa damu na dawa sawa na kuganda kwingine kwa damu kunaweza kuwa na athari mbaya sana—na watu wachache walifariki— kwa sababu damu yao iliyoganda haikutibiwa na dawa sahihi. Hakujakuwa na uhusiano wowote na kuganda kwa damu na chanjo za mRNA (Pfizer au Moderna).

Hakujakuwa na vifo kutokana na athari yoyote (hata zile nadra) kwa chanjo za mRNA (Pfizer na Moderna). Pfizer ndio chanjo pekee iliyoidhinishwa kwa watoto walio chini ya miaka 18. Chanjo ya Johnson & Johnson haijaidhinishwa kwa watoto walio chini ya miaka 18.



moderna

Johnson & Johnson

⁹ <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/safety/adverse-events.html>

Je, nani hapaswi kupata chanjo ya Pfizer ya COVID-19?

Chanjo ya Pfizer/BioNTech ya COVID-19 imeidhinishwa kwa watu wa umri wa miaka 12 na zaidi. Hupaswi kupata chanjo hii ikiwa:

- Alikuwa na athari kali ya mzio baada ya dozi ya 1 ya chanjo.
- Alikuwa na athari kali ya mzio kutokana na [kiungo](#) chochote kwenye chanjo.



Zungumza na daktari wako kabla ya kupata chanjo ya COVID-19 ikiwa alikuwa na athari ya mzio baada ya muda mfupi kwa dozi ya 1 ya chanjo ya COVID-19, au athari ya mzio kwa aina nyingine ya chanjo au tiba ya sindano ya ugonjwa mwingine, hata ikiwa haikuwa kali.

Unaweza kupata chanjo hata ikiwa una historia ya athari kali ya mzio ambayo haihusiani na chanjo au dawa za sindano, kama vile vyakula, mnyama kipenzi, sumu, mazingira, au mzio wa ulimbo wa mpira. Pia unaweza kupata chanjo ikiwa una historia ya mzio wa dawa za kumeza au historia ya familia ya athari mbaya ya mzio.¹⁰



Je, ninaweza kupata chanjo zingine kwa wakati mmoja na chanjo ya COVID-19?

Unapopata chanjo yako ya COVID-19, ni wakati mzuri kuhakikisha kuwa wewe na mtoto wako mmepata chanjo zingine. **Chanjo za COVID-19 na chanjo zingine zinaweza kutolewa siku hiyo hiyo, na hautalazimika kusubiri kupata chanjo ya COVID-19 ikiwa umepata aina tofauti ya chanjo katika siku 14 zilizopita.**¹¹

Muulize daktari wako kuhusu athari zinazoweza kama za kila chanjo, ili ujue ishara unazopaswa kuangalia. Inawezekana upate athari kutokana na chanjo ZOTE kwa wakati mmoja.




¹⁰ <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/recommendations/specific-groups/allergies.html>

¹¹ <https://www.cdc.gov/vaccines/covid-19/info-by-product/clinical-considerations.html#Coadministration>

Je, ninapaswa kuripoti athari yoyote nitapata baada ya kupata chanjo ya COVID-19?

Ikiwa unadhani umepata athari baada ya kupata chanjo, unaweza kuripoti kwa [Mfumo wa Kuripoti Tukio Baya la Chanjo \(VAERS\)](#) wa CDC. Unaweza pia kumwomba daktari wako kuripoti kwa VAERS kwa niaba yako. VAERS husaidia wanasayansi na wataalam wa matibabu kugundua haraka mitindo isiyoy kawaida au isiyotarajiwa ya matatizo ya kiafya (pia inaitwa “matukio mabaya”) ambayo yanaweza kuashiria matatizo ya usalama yanayowezekana na chanjo.



Jisajili na V-safe

V-safe ni nyenzo ya mtandaoni inayokuwezesha kufahamisha CDC ikiwa utapata athari zozote baada ya kupokea chanjo ya COVID-19. Pia unaweza kupata makumbusho ikiwa unahitaji dozi ya 2. Pata maelezo zaidi kuhusu v-safe kupitia www.cdc.gov/vsafe.



5 <https://www.cdc.gov/vaccines/covid-19/info-by-product/clinical-considerations.html#Coadministration>

6 <https://www.cdc.gov/vaccinesafety/concerns/multiple-vaccines-immunity.html>